

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 64 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JUNI 2026

TSC YAFANYA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI, YAJIPANGA UPYA KUIMARISHA HUDUMA KWA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao kazi cha tathmini ya mwisho ya Mpango Mkakati wa 2021/22–2025/26 tarehe 5 Mei, 2026 mjini Singida.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tumia e-Mrejesho na Njia Nyingine Kusaidia Kuboresha Huduma za TSC

Katika mazingira ya sasa ambapo Serikali inaendelea kuboresha huduma kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano, ushiriki wa wadau katika kutoa mrejesho ni jambo muhimu katika kuongeza uwajibikaji na ubora wa huduma zinazotolewa. Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa taasisi zinazoweka kipaumbele katika kusikiliza maoni, malalamiko, mapendekezo, maswali na pongezi kutoka kwa walimu na wadau wake ili kuendelea kuboresha huduma.

Miongoni mwa mifumo inayowawezesha wadau kuwasilisha mrejesho kwa urahisi ni Mfumo wa e-Mrejesho wa Serikali. Kupitia mfumo huo, mdau anaweza kuwasilisha hoja zake kwa kutumia tovuti ya e-Mrejesho, simu janja, huduma ya USSD kupitia *152*00# pamoja na Kituo cha Huduma kwa Wateja. Mfumo huu umeondoa vikwazo vya umbali na muda kwa kuwa unamwezesha mdau kuwasilisha mrejesho kutoka eneo lolote na kufuatilia hatua zinazochukuliwa.

Hata hivyo, e-Mrejesho si njia pekee inayopokea maoni ya wadau wa TSC. Tume imeendelea kuweka mazingira rafiki ya mawasiliano kupitia Mfumo wa TSCMIS, tovuti rasmi ya Tume, kurasa za mitandao ya kijamii, simu za ofisi, baruapepe pamoja na ofisi zake

zilizopo katika ngazi mbalimbali nchini. Upatikanaji wa njia hizi nyingi unaonesha dhamira ya Tume ya kuhakikisha kila mdau anapata nafasi ya kusikilizwa na kuhudumiwa kwa wakati.

Ni muhimu kutambua kuwa ubora wa huduma za umma haujengwi na taasisi pekee bali pia na ushiriki wa wananchi na wadau wanaozitumia huduma hizo. Mwalimu anayekutana na changamoto, anayehitaji ufafanuzi wa jambo fulani, mwenye pendekezo la kuboresha huduma au anayependa kutoa pongezi kwa huduma nzuri anapaswa kutumia fursa hizi za mawasiliano. Mrejesho unaotolewa leo unaweza kuwa chanzo cha suluhisho litakalowanufaisha walimu wengi kesho.

Kwa hiyo, Tume ya Utumishi wa Walimu inawahimiza walimu na wadau wote wa sekta ya elimu kutumia kikamilifu Mfumo wa e-Mrejesho pamoja na njia nyingine rasmi zilizowekwa kwa ajili ya kuwasilisha maoni, malalamiko, mapendekezo, maswali na pongezi. Sauti ya mdau ina thamani kubwa katika kuboresha huduma. Kadiri mrejesho unavyotolewa kwa wakati na kupitia njia sahihi, ndivyo inavyokuwa rahisi zaidi kwa Tume kuchukua hatua stahiki na kuendelea kuboresha huduma kwa manufaa ya walimu na wananchi kwa ujumla.

KATUNI

e-Mrejesho

NATAKA
KUWASILISHA
MAONI, MALALAMIKO
MAPENDEKEZO, MASWALI
NA PONGEZI KWA TUME
YA UTUMISHI WA WALIMU
e-Mrejesho NDIO
NJIA SAHIHI

HAKIKA!
HUU MFUMO
UNATURAHISISHA
SANA KUWASILISHA
MREJESHO WETU!
UMEONDOA VIKWAZO
VYA UMBALI NA
MUDA



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC YAFANYA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI, YAJIPANGA UPYA KUIMARISHA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Singida.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza tathmini ya kina ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa mwaka 2021/22–2025/26, huku ikiweka mkazo katika kuoanisha mipango yake na vipaumbele vya taifa pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

Akifungua kikao kazi hicho tarehe 5 Mei, 2026 mjini Singida, Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama alisema mapitio hayo yanalenga kuchanganua utekelezaji wa mpango uliopita, kubaini mafanikio, changamoto na kuweka msingi wa Mpango Mkakati mpya wa mwaka 2026/27–2030/31.

Alisisitiza kuwa mipango ya Tume lazima iendane na mwelekeo mpana wa maendeleo ya nchi, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, pamoja na Sera, Sheria na Mipango ya Sekta ya Elimu ili kuhakikisha taasisi hiyo inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Katika kusesitiza uwajibikaji, Mwl. Nkwama aliwataka watumishi wa Tume kuhakikisha haki za walimu zinashughulikiwa kwa wakati, alitaja masuala ya uthibitisho kazini, upandishaji madaraja na stahiki nyingine kuwa ni maeneo yanayohitaji umakini mkubwa katika



Mchumi Mkuu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Elia Malaki akitoa neno la kumkaribisha Katibu wa Tume kufungua kikao kazi hicho cha tathmini ya Mpango Mkakati.

upangaji na utekelezaji wa mipango.

Aidha, alionya dhidi ya urasimu usio wa lazima unaoweza kuchelewesha huduma, alibainisha kuwa hali hiyo inaweza kuathiri taswira ya juhudi za serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika

kuboresha sekta ya elimu.

Sambamba na hilo, aliwataka watumishi kuwa mfano wa maadili kwa walimu wanaowasimamia, pamoja na kuimarisha utamaduni wa kushirikishana katika kufanya kazi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Katika kuonesha mwenendo wa utekelezaji wa mpango unaofanyiwa tathmini, baadhi ya takwimu zilizotajwa ni pamoja na ajira na usajili wa walimu 67,352, kupandishwa madaraja kwa walimu kwa vibali 545,395 vilivyotolewa na Serikali, pamoja na kushughulikiwa kwa mashauri ya nidhamu 4,930 na rufaa 327.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa tathmini hiyo si ya kujipongeza bali ni fursa ya kujifunza na kuboresha utendaji wa taasisi kwa kuzingatia takwimu na mahitaji halisi ya sekta ya elimu.

Kwa upande mwingine, aliwahimiza watumishi wa Tume kuwaelimisha walimu kuhusu wajibu na haki zao kwa kusoma na kuzingatia nyaraka za kiutumishi, hatua itakayosaidia kuongeza uelewa na kupunguza changamoto zisizo za lazima kazini.



Mwezeshaaji kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dkt. Mzwageni akishiriki katika ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 5 Mei, 2026 mjini Singida.

TSC YAFANYA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI, YAJIPANGA UPYA KUIMARISHA HUDUMA KWA WALIMU



Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha tathmini ya Mpango Mkakati wa TSC wakifuatilia hotuba ya Katibu wa Tume (hayupo pichani).



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi hicho tarehe 5 Mei, 2026 mjini Singida.

e-MREJESHO: DARAJA JIPYA LA MAWASILIANO KATI YA TSC NA WADAU WAKE

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katika zama za mageuzi ya kidijitali, taasisi za umma zinaendelea kutumia teknolojia kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Miongoni mwa mifumo inayochangia kuimarisha uwazi, uwajibikaji na mawasiliano kati ya Serikali na wananchi ni Mfumo wa e-Mrejesho.

Kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), mfumo huu ni fursa muhimu inayowawezesha walimu na wadau wengine wa sekta ya elimu kuwasilisha maoni, malalamiko, mapendekezo, maswali na pongezi kuhusu huduma zinazotolewa na Tume kwa urahisi zaidi na kwa wakati.

Kwa miaka mingi, wadau walilazimika kutembelea ofisi za TSC au kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ambazo wakati mwingine zilihitaji muda na gharama zaidi. Kupitia mfumo wa e-Mrejesho, huduma hiyo imeboreshwa kwa kuwezesha wadau kuwasilisha hoja zao kwa njia za kidijitali na kufuatilia hatua zinazochukuliwa hadi kupata majibu.

Mfumo huu una manufaa makubwa kwa walimu ambao ndio wadau wakuu wa Tume. Mwalimu mwenye swali

kuhusu masuala ya utumishi, anayehitaji ufafanuzi wa jambo fulani au anayekutana na changamoto katika huduma anaweza kuwasilisha taarifa kupitia mfumo na kupata mrejesho bila ulazima wa kusafiri umbali mrefu kufika ofisini.

Aidha, e-Mrejesho unatoa fursa kwa walimu kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha huduma zinazotolewa na Tume. Kupitia maoni hayo, TSC inaweza kutambua maeneo yanayohitaji maboresho na kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

Faida nyingine kubwa ya mfumo huu ni kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa huduma. Kila hoja inayowasilishwa huingizwa katika mfumo na kufuatiliwa hadi itakapopatiwa ufumbuzi au majibu. Hali hii huongeza uwazi na kupunguza uwezekano wa hoja za wadau kupotea au kutopatiwa majibu kwa wakati.

Kwa upande wa TSC, mfumo wa e-Mrejesho ni nyenzo muhimu ya kupima kiwango cha kuridhika kwa wadau wake. Kupitia taarifa zinazokusanywa, Tume inaweza kufahamu changamoto zinazojitokeza mara kwa mara, kutambua mahitaji ya wadau na kupanga

mikakati bora ya kuboresha huduma.

Vilevile, mfumo huu unatoa nafasi kwa wananchi na wadau wengine wa elimu kutoa pongezi pale wanaporidhishwa na huduma wanazopata. Pongezi hizo ni sehemu muhimu ya kutambua mafanikio yaliyopatikana na kuwapa motisha watumishi wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Katika dunia ya sasa ambapo huduma nyingi zinahamia kwenye mifumo ya kidijitali, ushiriki wa wadau katika matumizi ya e-Mrejesho ni jambo muhimu. Kadri walimu na wananchi wanavyoutumia mfumo huo, ndivyo TSC inavyopata fursa kubwa zaidi ya kuboresha huduma zake kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wadau wake.

Kwa ujumla, Mfumo wa e-Mrejesho si tu njia ya kuwasilisha malalamiko au maoni, bali ni daraja muhimu linalounganisha Tume ya Utumishi wa Walimu na wadau wake. Kupitia mfumo huu, mawasiliano yanakuwa rahisi, huduma zinaboreshwa na uwajibikaji unaimarika, jambo linalochangia kujenga taasisi yenye kuwasikiliza na kuwahudumia wadau wake kwa ufanisi zaidi.

PROF. SHEMDOE ASISITIZA USIMAMIZI BORA WA ELIMU NA MIKAKATI YA KUINUA UFAULU

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Profesa Riziki Shemdoe, amewataka viongozi na watendaji wa sekta ya elimu nchini kuendelea kusimamia kwa ufanisi maendeleo ya taaluma kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari.

Profesa Shemdoe alitoa kauli hiyo jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliolenga kutathmini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo na mikakati ya kuendelea kuboresha kiwango cha ufaulu mkoani humo.

Akizungumza katika mkutano huo, Profesa Shemdoe aliwataka viongozi wanaosimamia elimu kuwa wabunifu, waadilifu na wenye kujituma ili kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya elimu.

Aliupongeza Mkoa wa Dodoma kwa mafanikio yake katika matokeo ya Mtihamu wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2025 na kuutaja ubunifu wa viongozi wa elimu kuwa miongoni mwa sababu zilizochangia mafanikio hayo.

“Mkoa wa Dodoma umeonesha kuwa mafanikio yanawezekana pale ambapo viongozi wa elimu, walimu na wadau wanashirikiana kwa karibu katika kutekeleza mikakati ya kuinua kiwango cha elimu,” alisema.

Profesa Shemdoe pia alikemea vitendo vya utoaji wa adhabu kwa wanafunzi kinyume na miongozo iliyowekwa na Serikali, akisema tabia hiyo imekuwa ikichangia baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo au kuwa watoro.

Aliwataka walimu na viongozi wa shule kuzingatia kikamilifu miongozo ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI katika kushughulikia nidhamu ya wanafunzi.

Katika hatua nyingine, Waziri huyo aliwataka viongozi wa mikoa na wilaya kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hususan ile ya elimu, ili kuhakikisha thamani ya fedha inayotolewa na Serikali inaonekana katika ubora wa miundombinu inayojengwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Prof. Riziki Shemdoe, akikagua mabanda ya maonesho ya taasisi mbalimbali za elimu kabla ya kufungua Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliofanyika jijini Dodoma, ukilenga kutathmini mafanikio yaliyopatikana, kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi mkoani humo.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, vyoo, mabweni na majengo mengine ya elimu yanayolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Profesa Shemdoe pia alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, kwa ubunifu wa kutoa motisha kwa walimu 34 na maafisa wawili wa elimu waliopata fursa ya kwenda nchini Korea Kusini kujifunza mbinu bora za usimamizi wa elimu.

Alisema hatua hiyo ni motisha muhimu kwa walimu na inaweza kuchangia kuongeza ari ya kazi pamoja na kuboresha matokeo ya wanafunzi.

Waziri huyo alikemea pia vitendo vya ubaguzi dhidi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum vinavyofanywa na baadhi ya shule kwa kuhofia kuathiri wastani wa ufaulu wa shule husika.

Aliwataka viongozi wa elimu na walimu kuhakikisha wanafunzi hao wanapatiwa maandalizi stahiki na mazingira rafiki yatakayowawezesha kufanya vizuri katika masomo na mitihani yao.

Aidha, Profesa Shemdoe alizitaka mamlaka za elimu kuanza mapema maandalizi ya kupokea ongezeko la wanafunzi watakojiunga na elimu ya sekondari mwaka 2028 kutokana na mabadiliko ya mfumo wa elimu yatakayosababisha wanafunzi wa

madarasa ya tano na sita ya mwaka 2026 kuanza kidato cha kwanza kwa wakati mmoja.

Alisema maandalizi hayo yahusishe ujenzi wa shule mpya, kuongeza vyumba vya madarasa, kutengeneza madawati pamoja na kuongeza miundombinu ya vyoo ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mazingira bora ya kujifunzia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, alisema mkoa huo umeandika historia mpya baada ya kushika nafasi ya pili kitaifa katika matokeo ya mitihani mwaka 2025.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa mikakati madhubuti, ushirikiano wa wadau wa elimu pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa majukumu katika ngazi zote.

Mhe. Senyamule alisema wadau wa elimu walioshiriki mkutano huo wameazimia kuhakikisha maazimio na mikakati inayopangwa inatekelezwa kwa vitendo ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuboresha zaidi sekta ya elimu katika Mkoa wa Dodoma.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa sekta ya elimu, wakiwemo maafisa elimu, walimu, wadau wa maendeleo pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwalimu Paulina Nkwama.

PROF. SHEMDOE ASISITIZA USIMAMIZI BORA WA ELIMU NA MIKAKATI YA KUINUA UFAULU



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Prof. Riziki Shemdoe, akikagua mabanda ya maonesho ya taasisi mbalimbali za elimu kabla ya kufungua Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliofanyika jijini Dodoma, ukilenga kutathmini mafanikio yaliyopatikana, kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kuendelea kuinua kizwango cha ufaulu wa wanafunzi mkoani humo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Prof. Riziki Shemdoe, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliofanyika jijini Dodoma kwa lengo la kutathmini mafanikio ya sekta ya elimu, kujadili changamoto na kuweka mikakati ya kuimarisha ufaulu wa wanafunzi katika mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, akitoa salamu za Mkoa wakati wa Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliojadili mafanikio, changamoto na mikakati ya kuendelea kuboresha utoaji wa elimu na kuongeza kizwango cha ufaulu wa wanafunzi mkoani humo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Prof. Riziki Shemdoe (kulia), akimkabidhi mmoja wa walimu 34 tiketi ya ndege kwa ajili ya safari ya mafunzo nchini Korea Kusini, yatakatayowajengea uwezo katika usimamizi bora wa elimu na uongozi wa taasisi za elimu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akiwasalimu washiriki wa Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliofanyika kwa lengo la kutathmini mafanikio, kujadili changamoto na kuweka mikakati ya kuendelea kuinua ubora wa elimu na ufaulu wa wanafunzi mkoani humo.

PROF. SHEMDOE ASISITIZA USIMAMIZI BORA WA ELIMU NA MIKAKATI YA KUINUA UFAULU



Baadhi ya walimu, viongozi wa elimu na wadau mbalimbali wakifuatilia mada wakati wa Mkutano wa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dodoma uliojadili mafanikio ya sekta ya elimu, changamoto zilizopo na mikakati ya kuendelea kuboresha matokeo ya wanafunzi katika mkoa huo.

FAHAMU TARATIBU ZA KUTHIBITISHA NA KUPANDISHA CHEO WALIMU

1. KUTHIBITISHA KAZINI WALIMU

Kanuni ya 5 (1) – (5) ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 zimeelekeza utaratibu wa kuwathibitisha kazini Walimu. Utaratibu unaelekeza kuwathibitisha kazini walimu ambao wamemudu majukumu ya kazi na kumwondoa kazini / kumwongezea muda Mwalimu ambao ameshindwa kumudu majukumu (hawajakidhi vigezo) baada ya kumaliza muda wa matazamia (Probationary Period) uliowekwa kisheria.

Vigezo na utaratibu wa kuthibitisha kazini Mwalimu

Mwalimu anapaswa kuthibitishwa kazini ndani ya miezi 12 tangu alipoajiriwa kwa mara ya kwanza kwenye Utumishi wa Umma; Mkuu wa Shule atatoa taarifa ya Utendaji wa Mwalimu katika kipindi cha Matazamia kwa kuzingatia Miezi mitatu kabla ya kumalizika kwa kipindi cha matazamia yaani (Miezi 12), Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika itapeleka tathmini na mapendekezo ya Walimu waliokidhi vigezo kwenye Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya.

Tume ngazi ya Wilaya itachambua na kuwasilisha kwenye Kikao cha Kamati ya Wilaya mapendekezo ya walimu waliokidhi vigezo na ambao wanastahili kuthibitishwa kazini na Kamati ya Wilaya itatoa uamuzi iwapo walimu husika wathibitishwe kazini au kipindi cha matazamia kiongezwe ili kumpa Mwalimu nafasi ya kujirekebisha au ajira yake isitishwe.

Mwalimu atajulishwa kwa barua juu ya uamuzi uliofikiwa. Iwapo Mwalimu atakuwa ameongezewa muda wa kipindi cha matazamia, muda huo haupaswi kuzidi miezi sita (6). Barua ya kuthibitishwa kazini izingatiwe.

Mwalimu aliyepewa muda wa nyongeza akishindwa kumudu majukumu ndani ya muda ulioongezwa, Kamati ya Wilaya itasitisha ajira yake baada ya kupokea kusudio la mwajiri la kuvunja mkataba.

2. UPANDISHAJI VYEO WALIMU

Kanuni Na. 8 ya Kanuni za Utumishi wa Walimu za Mwaka, 2016 imefafanua sifa zinazotakiwa ili mwalimu aweze kupandishwa cheo. Aidha, Waraka Na. 1 wa Mwaka 2014 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaohusu utaratibu wa kupandisha cheo Watumishi wa Umma wakiwemo Walimu umeelekeza utaratibu wa kuzingatiwa katika kupandisha cheo.

Mambo muhimu ya kuzingatiwa ni pamoja na uwepo wa Muundo wa Kada ya Mwalimu, uwepo wa Tange iliyohuishwa, uwepo wa Bajeti ya mishahara na Ikama iliyoidhinishwa.

Vilevile, Mwalimu anayepandishwa cheo lazima awe amethibitishwa kazini, hatakiwi kuwa na tuhuma yoyote ya kinidhamu, awe na utendaji kazi mzuri uliopimwa katikali wa Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS) kwa kipindi kisichopungua miaka Mitatu na

awe na uzoefu wa kutosha katika cheo anachokitumikia kwa kadri maelekezo yatavyotolewa na Serikali.

Utaratibu wa Kupandisha vyeo Walimu

Utaratibu wa kupandisha vyeo walimu utanza kwa Mkuu wa Shule atawasilisha taarifa za utendaji wa kazi wa Mwalimu kwa Mwajiri, Mwajiri akiridhika na taarifa ya utendaji wa Mwalimu, kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) ataandaa makisio ya Ikama na bajeti ya mwaka husika kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Mamlaka husika.

Baada ya kupokea Ikama na kibali, Mwajiri atawasilisha Orodha yamapendekezo ya wanaostahili kupanda cheo katika Ofisi ya Tume ngazi ya Wilaya, Tume ngazi ya Wilaya itapitia mapendekezo yaliyowasilishwa ili kujiridhisha kwa kupitia Tange, Muundo wa Kada ya walimu, Maelekezo/ Miongozo iliyotolewa pamoja na Nyaraka nyingine.

Katibu Msaidizi atawasilisha mapendekezo kwenye Kamati ya Wilaya ambayo baada ya kuridhika atapandisha cheo mwalimu, Mwalimu ataandikiwa barua ya kupandacheo na Katibu wa Kamati ya Wilaya ambayo itapitishwa na Mwajiri wa Mwalimu husika, kwa kuzingatia fomati iliyotolewa, Mwalimu ambaye hatapandishwa cheo kwasababu zozote ingawa alikasimiwa, atajulishwa kwa barua kwa fomati iliyotolewa na Mwajiri ataingiza kwenye mfumo barua ya cheo cha mwalimu na atarekebisha mishahara wa Mwalimu aliyepandishwa cheo.

NAIBU KATIBU MKUU MWAMBENE AKUTANA NA MAKAMISHNA WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Morogoro

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Bw. Atupele Mwambene, amekutana na kufanya mazungumzo na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mjini Morogoro kwa lengo la kujadili utekelezaji wa majukumu ya Tume na namna ya kuimarisha huduma kwa walimu nchini.

Katika kikao hicho, viongozi hao walijadiliana masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Tume, ikiwemo usimamizi wa mashauri ya rufaa za walimu na utatuzi wa changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa huduma.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Bw. Mwambene alisema ameridhishwa na namna Tume inavyotekeleza majukumu yake, hususan katika kushughulikia rufaa zinazowasilishwa na walimu wanaopinga maamuzi ya mamlaka za nidhamu katika ngazi za wilaya.

“Nimepata fursa ya kujionea namna Tume inavyosimamia usikilizaji wa rufaa za walimu na nimefurahishwa na utaratibu uliowekwa katika kuhakikisha haki inatendeka kwa walimu wanaowasilisha rufaa zao,” alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaendelea kushirikiana kwa karibu na Menejimenti ya Tume katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoweza kuathiri utekelezaji wa majukumu yake.

“Mimi ni sehemu ya taasisi zinazohudumia sekta ya elimu, hivyo nimeona ni muhimu kufika hapa kujionea utekelezaji wa majukumu yenu. Tume kuwa na mawasiliano ya karibu na Menejimenti ya Tume katika kushughulikia masuala mbalimbali yanayowahusu walimu,” alisisitiza.

Bw. Mwambene aliipongeza TSC kwa kazi kubwa inayofanya ya kusimamia masuala ya utumishi wa walimu na kuitaka kuendelea kuwa karibu na walimu kwa kushughulikia changamoto zao kwa wakati.

Awali, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Profesa Masoud Hadi Muruke, alimshukuru Naibu Katibu Mkuu kwa kutenga muda wa kukutana na Makamishna pamoja na watumishi wa Tume.

Profesa Muruke alisema ziara hiyo imeipa Tume fursa ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu yake pamoja na kupata mawazo yatakayosaidia kuongeza ufanisi wa huduma zinazotolewa kwa walimu nchini.

Alieleza kuwa Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu katika kuboresha mazingira ya kazi na huduma zinazotolewa kwa walimu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Bw. Atupele Mwambene (katikati), akizungumza na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa kikao cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Tume na huduma zinazotolewa kwa walimu mjini Morogoro. Kulia ni Mwenyekiti wa TSC, Profesa Masoud Hadi Muruke, na kushoto ni Katibu wa Tume, Mwalimu Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Profesa Masoud Hadi Muruke (kulia), akitoa maelezo ya utangulizi kabla ya kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Bw. Atupele Mwambene (katikati), kuzungumza na Makamishna wa Tume mjini Morogoro. Kushoto ni Katibu wa Tume, Mwalimu Paulina Nkwama.

NAIBU KATIBU MKUU MWAMBENE AKUTANA NA MAKAMISHNA WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwalimu Paulina Nkwama, akitoa salamu za Tume wakati wa kikao cha Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Bw. Atupele Mwambene, na Makamishna wa Tume mjini Morogoro.



Baadhi ya Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakifuatilia mazungumzo wakati wa kikao cha Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Bw. Atupele Mwambene, kilichofanyika mjini Morogoro.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Bw. Atupele Mwambene (katikati, mstari wa mbele), akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu baada ya kikao cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Tume na huduma kwa walimu mjini Morogoro.

WAALIMU 61 WA SHULE ZA SEKONDARI ROMBO WAPATIWA MAFUNZO ELEKEZI YA UTUMISHI WA UMMA

Na mwandishi wetu – Rombo

Mafunzo elekezi kwa walimu walioajiriwa katika Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yametolewa kwa walimu 61 wa shule za sekondari za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo. Mafunzo hayo yamefanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo na kuendeshwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya hiyo Mwl. Zema Jamali. Mgeni rasmi katika mafunzo hayo ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Rombo Bi. Johari Athumani.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Raymond Mwangwala, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo Ndugu Godwin Chacha, Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Mwl. Christina Marwa pamoja na wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo TAKUKURU,



Usalama, Elimu Msingi, CWT, Udhhibiti Ubora wa Shule, Ustawi wa Jamii na taasisi za fedha kama CRDB na NMB.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali zimewasilishwa na wawezeshaji akiwemo Afisa Ajira wa TSC Wilaya Bi. Rose Mawole pamoja na Afisa Nidhamu Bi. Kadis Soda

zikilenga kuwaandaa walimu hao kuendana na matarajio ya sekta ya elimu na utumishi kwa ujumla.

Akizungumza katika mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Raymond Mwangwala amewataka walimu hao kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na nidhamu huku wakizingatia maadili ya taaluma yao ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya elimu wilayani humo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo Ndugu Godwin Chacha amewakaribisha walimu hao wilayani humo na kuahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, ameeleza kuwa changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo ucheleweshaji wa malipo ya fedha za kujikimu kwa baadhi yao zinaendelea kufanyiwa kazi na wahusika ili zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Nao walimu waliopatiwa mafunzo hayo wakizungumza mbele ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo wamewashukuru waandaji wa mafunzo hayo na kuahidi kufanya kazi kwa bidii na weledi wakizingatia maadili ya Utumishi wa Umma



WAALIMU 61 WA SHULE ZA SEKONDARI ROMBO WAPATIWA MAFUNZO ELEKEZI YA UTUMISHI WA UMMA



KAMATI YA TSC YAPITIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu imefanya kikao chake Mei 12, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma, kwa lengo la kupitia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume pamoja na kujadili namna ya kuendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa walimu nchini.

Kikao hicho kiliongozwa na mmoja wa Makamishna

wa Tume, Bw. Aggrey Mleli, huku Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, akihudumu kama Katibu wa kikao. Aidha, Kamishna wa Tume, Mwl. Lameck Mahewa alikuwa mjumbe wa kikao hicho kilichohudhuriwa pia na wajumbe wa Menejimenti ya Tume.

Katika kikao hicho, masuala mbalimbali yanayohusu utawala, usimamizi wa fedha, utafiti pamoja na elimu kwa umma yalijadiliwa huku msisitizo ukiwekwa katika kuendelea kuimarisha mifumo ya utendaji kazi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Pamoja na hilo, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara na Vitengo vya Tume kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuangalia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa.

Majadiliano hayo pia yaligusia umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu majukumu ya Tume na haki pamoja na wajibu wa walimu, hatua inayolenga kuongeza uelewa na kuimarisha ushirikiano katika sekta ya elimu.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Bw. Aggrey Mleli alisisitiza umuhimu wa ushirikiano na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ili kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa walimu zinaendelea kuimarika na kuleta matokeo chanya katika sekta ya elimu nchini.

Kikao hicho ni sehemu ya utaratibu wa Tume wa kufuatilia utekelezaji wa majukumu yake na kufanya tathmini ya hatua zinazochukuliwa katika kuboresha utumishi wa walimu nchini.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Aggrey Mleli (Katikati) akiongoza kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma kilichofanyika tarehe 12 Mei, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma. Pichani, upande wa kulia ni Katibu wa Kikao ambaye pia ni Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama na kushoto Mjumbe wa kikao na Kamishna wa Tume, Mwl. Lameck Mahewa.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akitoa ufafanuzi wakati wa kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma tarehe 12 Mei, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

KAMATI YA TSC YAPITIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA HUDUMA KWA WALIMU



Washiriki wa kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma cha TSC kilichofanyika Dodoma wakikwa kwenye kikao hicho.

WATUMISHI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAJENGEWA UWEZO KUHUUSU USIMAMIZI WA MFUMO WA e-UTENDAJI

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamejengewa uwezo kuhusu usimamizi na matumizi sahihi ya Mfumo wa e-Utendaji katika mafunzo yaliyotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji, ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Akitoa mafunzo hayo jijini Dodoma, Mchambuzi Kazi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Shomi Mongi, alisema Mfumo wa e-Utendaji ni nyenzo muhimu katika kupima na kufuatilia utendaji wa watumishi wa umma kwa kuzingatia malengo na majukumu waliyopewa.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuongeza uelewa wa watumishi kuhusu matumizi sahihi ya Mfumo huo ili kuboresha uwajibikaji binafsi na Taasisi kwa ujumla.

Bi. Mongi aliwataka Wakuu wa Idara, Sehemu na Vitengo kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa kufanya tathmini ya kina ya utendaji wa watumishi wanaowasimamia kabla ya kuidhinisha taarifa zao kwenye mfumo.

"Ni muhimu kwa wasimamizi kufanya tathmini kwa kuzingatia utendaji halisi wa mtumishi na kutoa alama zinazostahili kulingana na utekelezaji wa majukumu yake. Hii itasaidia kuimarisha uwazi, uwajibikaji na tija katika Utumishi wa Umma," alisema.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya mfumo huo katika kuimarisha utamaduni wa kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo na malengo ya taasisi.


Katika hatua nyingine, Bi. Mongi aliipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa namna inavyotekeleza Mfumo wa e-Utendaji na kuhimiza watumishi kuendelea kuutumia kwa ufanisi ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma.

Mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utendaji kazi katika utumishi wa umma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, hatua inayolenga kuongeza uwajibikaji na ubora wa huduma kwa wananchi.



Baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakifuatilia mafunzo kuhusu usimamizi na matumizi sahihi ya Mfumo wa e-Utendaji yaliyofanyika jijini Dodoma.

WATUMISHI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAJENGEWA UWEZO KUHUSU USIMAMIZI WA MFUMO WA e-UTENDAJI



Baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika picha ya pamoja na mwezeshaji wa mafunzo ya usimamizi sahihi wa Mfumo wa e-Utumishi kutoka Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (wa kwanza kutoka kulia kwa waliokaa) yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

WALIMU KONDOA WAIPONGEZA TSC KWA KUIMARISHA MATUMIZI YA MFUMO WA TSCMIS

Na Mwandishi Wetu – Kondoia.

Walimu wa Wilaya ya Kondoia mkoani Dodoma wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kuboresha na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa TSCMIS, ambao umechangia kurahisisha utoaji wa huduma na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu.

Pongezi hizo zimetolewa wakati wa mahojiano yaliyofanywa na Afisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano cha TSC Makao Makuu alipotembelea Shule ya Msingi Iboni iliyopo Kata ya Chemchem, Wilaya ya Kondoia, kwa lengo la kupata maoni ya walimu kuhusu huduma zinazotolewa na Tume pamoja na matumizi ya mfumo huo.

Akizungumza katika mahojiano hayo, Mwalimu Ashura Bakari alisema mfumo wa TSCMIS umeleta mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma kwa walimu kwa kurahisisha usajili wa walimu, usimamizi wa mikataba, ufuatiliaji wa upandaji wa vyeo pamoja na uwasilishaji na utatuzi wa changamoto mbalimbali kwa wakati.

“Kwa sasa walimu wanaweza kuwasilisha changamoto zao, kufuatilia maombi mbalimbali na kupata mrejesho kwa wakati kupitia mfumo huu. Hii imeongeza ufanisi na kurahisisha mawasiliano kati ya walimu na TSC,” alisema.

Aidha, alieleza kuwa mfumo huo umeimarisha mawasiliano kati ya shule, walimu, TSC ngazi ya wilaya na Makao Makuu, huku akiishauri Tume kuendelea kutoa mafunzo na kuwafikia walimu zaidi ili kuongeza uelewa na matumizi sahihi ya mfumo huo.



Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kondoia, Mwalimu Geoffrey Lugano, akizungumza kuhusu mchango wa maboresho ya mfumo wa TSCMIS katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Kwa upande wake, Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kondoia, Mwalimu Geoffrey Lugano, alisema maboresho ya TSCMIS yameongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu na kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wakati.

Alibainisha kuwa mfumo huo umechangia kupunguza muda wa kushughulikia hoja na changamoto za walimu, jambo linaloimarisha imani na kuridhika kwa walimu wanaohudumiwa na Tume.

Naye Mwalimu Joyce Olengiriki aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada zake za kuboresha maslahi ya walimu kupitia upandishaji wa vyeo, ulipaji wa stahiki mbalimbali pamoja na utatuzi wa changamoto zilizokuwa zikiathiri utendaji wao wa kazi.

“Hatua hizi zimeongeza ari na morali ya walimu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku,” alisema.

Katika mahojiano hayo, Mwalimu Suzana Lucas Palla wa Shule ya Sekondari Kwapakacha alisema ziara za mara kwa mara zinazofanywa na maafisa wa TSC wilayani humo zimekuwa na manufaa makubwa kwa walimu kwani zimeongeza fursa za kusikilizwa na kupatiwa ufumbuzi wa changamoto zao kwa wakati.

Alisema hali hiyo imechangia kurejesha utulivu na ari ya kazi miongoni mwa walimu tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo baadhi ya changamoto zilichelewa kupata ufumbuzi.



Mwalimu Ashura Bakari wa Shule ya Msingi Iboni, Wilaya ya Kondoia, akielezea namna mfumo wa TSCMIS ulivyorahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za Tume ya Utumishi wa Walimu.



Mwalimu Suzana Lucas Palla wa Shule ya Sekondari Kwapakacha akielezea manufaa ya ziara za maafisa wa TSC katika kutatua changamoto za walimu kwa wakati.

WALIMU KONDOA WAIPONGEZA TSC KWA KUIMARISHA MATUMIZI YA MFUMO WA TSCMIS

Kwa upande wake, Mwalimu Ferida Michael Chaula alisema miongozo inayotolewa na TSC kuhusu maadili na utekelezaji wa majukumu ya kazi imekuwa msaada mkubwa katika kuwawezesha walimu kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.



Mwalimu Ferida Michael Chaula akizungumzia umuhimu wa miongozo ya TSC katika kuimarisha maadili na uwajibikaji kazini miongoni mwa walimu

Naye Mwalimu Modest Hhayuma, ambaye ni mwajiriwa mpya, alieleza kuwa mafunzo elekezi na semina zinazotolewa na TSC zimechangia kuwaimarisha walimu wapya katika utekelezaji wa majukumu yao na kuwaepusha na makosa yanayoweza kusababisha mashauri au adhabu za kinidhamu.

Walimu hao kwa pamoja wameitaka TSC kuendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu nchini.



Mwalimu Modest Hhayuma akieleza jinsi mafunzo elekezi yanayotolewa na TSC yanavyowawezesha walimu wapya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.



Baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari Kwapakacha wakirwa katika picha ya pamoja na Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kondoa baada ya mazungumzo kuhusu huduma zinazotolewa na Tume.

WADAU WAKUTANA KUJADILI USHIRIKIANO KATIKA USHUGHULIKIAJI WA MAFAO NA MIRATHI YA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akifungua kikao kazi kilichowakutanisha wadau wanaoshughulikia masuala ya pensheni, mirathi na mikataba ya ajira za walimu, kilichofanyika tarehe 26 Mei 2026 jijini Dodoma.

Na mwandishi wetu – Dodoma.

Kikao kazi cha wadau wanaoshughulikia mafao yanayohusu mirathi, pensheni na mikataba maalum ya walimu kimefanyika tarehe 26 Mei, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC) jijini Dodoma kikiwa na lengo la kuimarisha ushirikiano na kuongeza ufanisi katika utoaji wa stahiki kwa wakati.

Mafao ya pensheni na mirathi yaliyojadiliwa katika kikao hicho ni yale yanayohusu walimu waliostaafu au kufariki kabla ya tarehe 1 Julai 2004, kwa kuwa hawapo kwenye mifumo ya sasa ya hifadhi ya jamii.

Aidha, eneo la mikataba linahusu

walimu wageni wakaazi pamoja na walimu walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45, ambao mikataba yao inashughulikiwa katika utaratibu maalum wa kiutumishi na malipo.

Akifungua kikao kazi hicho kilichoratibiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, alisema mafao hayo ni eneo nyeti linalogusa moja kwa moja ustawi wa walimu husika na familia zao, hivyo yanahitaji uratibu imara kati ya taasisi zote zinazohusika.

Ameeleza kuwa kikao hicho kimewakutanisha wadau kutoka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu, ili kujadili

namna bora ya kuboresha mchakato wa ushughulikiaji wa mafao hayo yanayolipwa kupitia Hazina baada ya taratibu za uhakiki kukamilika.

Mwl. Nkwama alisema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuweka kipaumbele katika ustawi wa watumishi wa umma, hususan katika kuhakikisha madai ya stahiki za watumishi yaliyotokana na mifumo ya awali yanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Ameongeza kuwa Tume inaendelea na jukumu la kupokea, kuhakiki na kuwasilisha majalada ya madai ya mafao kwa Hazina kupitia mfumo wa TPPS, baada ya kukamilika kwa uhakiki wa kitaalamu unaofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Aidha, amesisitiza kuwa mafao hayo ni ya kihistoria na yanawahusu walimu husika kulingana na masharti ya ajira na mifumo iliyokuwepo kipindi husika, hivyo yanapaswa kushughulikiwa kwa umakini ili kulinda haki za wanufaika wake.

Kwa ujumla, wadau wamesisitizwa kuimarisha ushirikiano wao ili kuhakikisha mchakato wa ushughulikiaji wa mafao na mirathi unakuwa wa haraka, sahihi na wenye tija, kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na kulinda heshima ya utumishi wa umma.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Fatuma Muya akitoa neno katika kikao kazi cha wadau wanaoshughulikia masuala ya pensheni, mirathi na mikataba ya ajira za walimu, kilichofanyika tarehe 26 Mei 2026 jijini Dodoma.

WADAU WAKUTANA KUJADILI USHIRIKIANO KATIKA USHUGHULIKIAJI WA MAFAO NA MIRATHI YA WALIMU



Washiriki wa kikao kazi kutoka Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (wenye tai zinazofanana) wakifuatilia mjadala katika kikao kazi cha wadau wanaoshughulikia masuala ya pensheni, mirathi na mikataba ya ajira za walimu, kilichofanyika tarehe 26 Mei 2026 jijini Dodoma.



Washiriki wa kikao kazi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa kwenye kikao kazi cha wadau wanaoshughulikia masuala ya pensheni, mirathi na mikataba ya ajira za walimu, kilichofanyika tarehe 26 Mei 2026 jijini Dodoma.

WILAYA YA KYELA YATOA USHUHUDA WA MAFANIKIO YA MIAKA 10 YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Kyela

Wilaya ya Kyela ni miongoni mwa maeneo yana yoshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 2016, kufuatia kutungwa kwa Sheria Na. 448 iliyoanzisha Tume hiyo kutoka iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD).

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela, Bw. Julius Mwambongela, miaka kumi ya uwepo wa TSC imeleta mabadiliko makubwa katika usimamizi wa utumishi wa walimu, utoaji wa huduma na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Alisema moja ya mafanikio makubwa ni kuboreshwa kwa muundo wa utendaji wa Tume ambapo kwa sasa mawasiliano kati ya Ofisi za Wilaya na Makao Makuu yanafanyika moja kwa moja, hali inayorahisisha utoaji wa maamuzi na utekelezaji wa majukumu kwa wakati.


"Katika mfumo wa sasa, mawasiliano na uratibu wa shughuli za Tume umeimarika zaidi kuliko ilivyokuwa kipindi cha TSD. Hii imesaidia kuongeza ufanisi na kuharakisha utoaji wa huduma kwa walimu," alisema.

Bw. Mwambongela alieleza kuwa maboresho hayo yamekwenda sambamba na kuimarishwa kwa upatikanaji wa rasilimali za uendeshaji wa ofisi za Tume katika ngazi ya wilaya, jambo lililosaidia kuboresha mazingira ya kazi na utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Aidha, alisema uwezeshaji wa maafisa wa Tume kufanya ziara za mara kwa mara katika shule umesaidia kuwafikia walimu moja kwa moja, kusikiliza changamoto zao, kutoa ufafanuzi kuhusu haki na wajibu wao pamoja na kuelimisha kuhusu maadili ya utumishi wa ualimu.

Kwa mujibu wa Bw. Mwambongela, hatua hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza mashauri ya kinidhamu katika Wilaya ya Kyela kutoka mashauri 21 mwaka 2016 hadi mashauri matano pekee mwaka 2026.

Aliongeza kuwa Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa Tume kwa kuweka muundo rasmi wa utumishi unaobainisha majukumu ya



Muonekano wa Ofisi ya iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) Wilaya ya Kyela kabla ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu mwaka 2016.



Muonekano wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela baada ya kufanyirwa maboresho ya miundombinu katika kipindi cha miaka 10 ya TSC.

kila afisa, jambo ambalo limeongeza uwajibikaji na kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu na wadau wengine.

Mafanikio mengine yaliyotajwa ni utekelezaji wa mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya ambayo huwasaidia kuelewa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa ualimu mapema wanapoanza kazi.

Kwa upande wa ushirikiano wa taasisi, Bw. Mwambongela alisema kuanzishwa kwa TSC kumeimarisha uratibu kati ya Tume na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan katika masuala ya upandishaji vyeo, mabadiliko ya kada na usimamizi wa maendeleo ya walimu.

Alifafanua kuwa kabla ya kuanzishwa kwa TSC kulikuwa na changamoto za uratibu kati ya taasisi mbalimbali zilizohusika na masuala ya walimu, jambo lililosababisha baadhi

ya maamuzi kuchelewa kutekelezwa na kuathiri huduma kwa walimu.

"Kwa sasa ushirikiano umeimarika na changamoto nyingi zilizokuwa zikiwakabili walimu katika masuala ya utumishi zinapatiwa ufumbuzi kwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali," alisema.

Akihitimisha mahojiano hayo, Bw. Mwambongela alisema kuwa katika kipindi cha miaka kumi ya TSC, kumekuwepo ongezeko la mshikamano miongoni mwa watumishi wa Tume, kuimarika kwa mazingira ya kazi pamoja na kuongezeka kwa ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Alisema mafanikio hayo yanaonesha mchango mkubwa wa Tume katika kuimarisha usimamizi wa utumishi wa walimu na kuboresha huduma kwa walimu nchini tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

WILAYA YA KYELA YATOA USHUHUDA WA MAFANIKIO YA MIAKA 10 YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Muonekano wa Ofisi ya iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) Wilaya ya Kyela kabla ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu mwaka 2016.

Muonekano wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela baada ya kufanyirwa maboresho ya miundombinu katika kipindi cha miaka 10 ya TSC.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela, Bw. Julius Mwambongela, akizungumza na walimu wa Kata ya Ipinda kuhusu masuala ya utumishi na maadili ya kazi.



Baadhi ya walimu wa Kata ya Ipinda wakifuatilia maelezo yaliyokuwa yakitolewa na viongozi wa Tume kuhusu haki, wajibu na maendeleo yao ya kiutumishi.

Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu Wilaya ya Kyela, Bw. Ibrahim John Ibrahim, akitoa elimu kwa walimu wa Kata ya Matema kuhusu masuala ya ajira na maendeleo ya utumishi.

MIAKA 10 YA TSC YALETA MAFANIKIO MAKUBWA KWA WALIMU WILAYANI MANYONI

Na Mwandishi Wetu, Manyoni

Wilaya ya Manyoni ni miongoni mwa maeneo yaliyoshuhudia maboresho makubwa katika usimamizi wa utumishi wa walimu tangu kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 2016.

Tume hiyo ilianzishwa kwa Sheria Na. 25 ya Mwaka 2015 na kuanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2016, ikichukua baadhi ya majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) chini ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Manyoni, Bw. Samora Nongere Juma, miaka 10 ya uwepo wa TSC imeleta mafanikio makubwa katika usimamizi wa masuala ya walimu, hususan katika kushughulikia rufaa za mashauri ya kinidhamu, upandishaji wa vyeo na maendeleo ya kiutumishi.

Alisema Tume imekuwa na mchango mkubwa katika uchambuzi wa walimu wanaostahili kupandishwa vyeo pamoja na kushughulikia changamoto za walimu waliokuwa wameachwa katika makundi yao ya rika.

"Kwa sasa walimu wengi wamepata haki zao za kiutumishi kwa wakati na changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika upandishaji wa vyeo

zimepungua kwa kiwango kikubwa," alisema.

Bw. Juma aliongeza kuwa TSC imeshiriki pia katika uchambuzi wa madai mbalimbali ya walimu, ikiwemo madeni ya mishahara na yasiyo ya mishahara, hatua iliyosaidia kuhakikisha walimu wengi wanapata stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Serikali.

Katika eneo la maadili ya utumishi, alisema uwepo wa Tume umechangia kuimarika kwa nidhamu ya kazi miongoni mwa walimu pamoja na kuongeza ufanisi katika usikilizaji na utatuzi wa mashauri ya kinidhamu.

Alifanua kuwa kupitia elimu ya mara kwa mara kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu, walimu wameendelea kuongeza uelewa wa wajibu wao na hivyo kupunguza migogoro inayotokana na ukiukwaji wa maadili ya kazi.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni utekelezaji wa mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya yanayowawezesha kuanza kazi wakiwa na uelewa wa kutosha kuhusu haki, wajibu na maadili ya utumishi wa umma.

Kwa upande wa ushirikiano, Bw. Juma alisema TSC imeimarisha mahusiano na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu, wakiwemo waajiri, vyama vya wafanyakazi na taasisi nyingine za Serikali, jambo ambalo limeongeza ufanisi katika kutatua

changamoto zinazowakabili walimu.

"Ushirikiano huu umewezesha kubadilishana taarifa kwa wakati na kujadili kwa pamoja masuala yanayohusu ustawi na maendeleo ya walimu," alisema.

Akizungumzia tofauti kati ya TSD na TSC, Bw. Juma alisema kuanzishwa kwa Tume kumeongeza uhuru na ufanisi katika kushughulikia masuala ya walimu kwa kuwa taasisi hiyo imejikita moja kwa moja katika usimamizi wa utumishi wa wao.

Aidha, aliipongeza Serikali kwa kuendelea kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake na kushauri kuendelea kuboreshwa kwa mifumo ya TEHAMA, hususan Mfumo wa TSCMIS, pamoja na kuimarishwa kwa mafunzo ya maadili ya utumishi kwa watumishi wa Tume na walimu.

Alisema Ofisi ya Tume Wilaya ya Manyoni itaendelea kuongeza kasi ya kushughulikia malalamiko na rufaa za walimu, kuimarisha huduma katika maeneo ya vijijini na kuendelea kushirikiana na wadau wa elimu ili kuhakikisha changamoto za walimu zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati.

Kwa ujumla, miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu imeacha alama chanya katika Wilaya ya Manyoni kwa kuimarisha usimamizi wa utumishi wa walimu, kuongeza ufanisi wa huduma na kuimarisha ustawi wa walimu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Manyoni, Bw. Samora Nongere Juma, akielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu